

MTIHANI WA KISWAHILI KIDATO CHA 2

JINA..... NAMBARI.....

SEHEMU A; INSHA ALAMA 20

Andika ratiba ya siku ya wazazi shuleni

SEHEMU YA B: UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

MAVAZI REKEBISHENI

Vazi njema kivaliwa, huongezeka heshima,
Staha mtu kapewa, poteendapo daima, Mavazi
duni si sawa, kina dada ninasema, Mavazi
rekebisheni usheratiumezidi.

Longi kwa nyuma kushika, na mapajani kubana,
Chupizilipowafika, dhahiri kuonekana,
Buremunaaibika, na kujishusha maana, Mavazi
rekebisheni, usheratiumezidi.

Kifuanikujikaza, maziwayaning'inie,
Kitu gani munawaza, hamna bahari nyie, Ni
ashikimwasambaza, sikizeniniwambie,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Msichana ni hatia, magotnikufichuka,
Hivyo basi kuvalia, rindalisoyafunika,
Huenda zusha hisia, maovuyakawafika, Mavazi
rekebisheni, usheratiumezidi.

Sitakosakuzitaja, skatimnazovaa,
Zaisha kwa mapaja, kikirikuchuchumaa,
Iko wazi nyonga moja, mkatouliyokaa, Mavazi
rekebisheni, usheratilumezidi.

Wazi nitawasomea, nguo hizi nguo gani?
Dada zetumwakosea, kuzivaahadharani, Ndizo
hizo huchochea, usherati mitaani, Mavazi
rekebisheni, usheratiumezidi.

Nguo chini zishusheni, mwilini mzipanue,
Heri kuingia deni, za heshima mnunue,
Kuigiza za kigeni, ni utumwamtambue, Mavazi
rekebisheni, usheratiumezidi.

Betيسانamaliza, kalamunaweka chini, Iwapo
wajiuliza, nakereketwa ni nini?
Ni stahanahimiza, sio wake kuhaini,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

MASWALI YA USHAIRI

(a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 2)

(b) Eleza vina vya beti za kwanza mbili (alama 2)

(c) Toa kibwagizo cha shairi hili kisha ufafanue maana yake. (alama 2)

(d) Eleza maana ya misamiati hii kama ilivyotumika katika ushairi. (alama 4)

Staha –

Dhahiri –

Shani –

Duni –

(e) Shairi hili liko katika bahari zipi? (alama 2)

(f) Uhuru wa mshairiunadhihirikavipi katika shairi hili? (Alama 3)

MATUMIZI YA LUGHA (AL 30)

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au si ghuna. (al 1)
/Z/

/K/
2. Eleza maana ya kiimbo. (al 1)
3. Eleza maana ya shadda. (al 1)
4. Eleza maana ya mofimu.(al 2)
5. Andika kwa wingi sentensi hizi. (Al.2)
 - i. Goti la mtoto liliumia.
 - ii. Ukwato wa ngamia ni mpana.
6. Bainisha nomino hizi ni za aina gani. (al.2)
 - i. Sukari.
 - ii. Mapenzi.
7. Tumiavivumishi vya sifa katika mabanokukamilisha sentensi zifuatazo. (al 2)
 - i. Mtoto Yule ni _____ (nene)
 - ii. Bei ya meli ni _____ mno (ghali)

8. Jazapengo kwa kiulizi sahihi kisha uandike sentensi kwa wingi (al 2) Ni mpishi _____ aliyepika.
9. Fafanua maana ya misemo ifuatayo. (al2)
- i. Kula mate.
10. Andika katika ukubwa. (al 2)
- i. Jiji hili litapanukaupesi.
 - ii. Jizeelililokosa adabu limekaripiwa.
11. Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya usemi halisi. (al 2)
- i. Ruhennialishauliwa na kasisiaache tabia mbaya.
 - ii. Mwalimu alimwabiapremjiafanye bidii katika masomo yake.
12. Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeshana. (al 2)
- i. Penda .
 - ii. Endesha.
13. Tambua kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo. (al 2)
- i. Anatembea kwa madaa kama tausi.
14. Kanusha sentensi zifuatazo. (Al) 2
- i. Mimi nilicheza.
 - ii. Wewe huchora.

15. Kamilisha methali zifuatazo ?(al 1)

i. Cha kuvunda. _____

16. Andika kinyume cha maneno yafuatayo. (al 2)

i. Tandika _____

ii. Umba _____

17. Pambanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. (al 2)

Naimba huku nafanya kazi. _____

ISIMU JAMII(ALAMA 5)

Eleza sifa za lugha ya hotelini

FASIHI SIMULIZI (al 10)

a) Taja aina nne za hadithi.

.

b) Eleza umuhimu wa hadithi.